# WAJIBU WA MJA KATIKA MAAMRISHO YA ALLAH

SHEIKH :

MUHAMMAD ABDULWAHAB ALLAH AMREHEMU

TARJAMA: UMMATI ABDALLAH , ABUU MUHAMMAD

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

مركز ابن عثيمين الإسلامي دودوما تنزانيا

**IBNU UTHAYMIN ISLAMIC CENTRE**

P.o Box 1984 Dodoma

E-Mail: ibnuthaymiindom @gmail.com

Website: www.ibnuthaymindom.or.tz

Phone: +255 765 713 116

P.o. Box 1984 Hazina, Dodoma.

# UTANGULIZI:

Sifa zote njema anastahiki ALLAH mola Mlezi wa Ulimwengu. Na sala na salamu ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad pamoja na watu wake na maswahaba wake wote na watakaowafuata wao kwa wema mpaka siku ya mwisho.

Baada ya utangulizi huo;

Hii ni Tarjama kwa Lugha ya Kiswahili kutoka katika maneno ya mwanazuoni Mtukufu Muhammad Ibnu Abdilwahaab Allah amrehemu yaliyomo kwenye risala yake fupi iitwayo (واجب العبد) .Kutokana na umuhimu wa kulelewa katika malezi ya elimu za wanazuoni wetu , tumeona tufanye tarjama hii ya Kiswahili ili tuweze kunufaika sote na faida kemkem zilizo ndani ya risala hii. Asili ya tarjama hii ni darsa za baada ya swala ya Adhuhuri zinazoendelea katika Markaz Ibnu Uthaymin, Masjid Saiid hapa jijini Dodoma ambapo risala hii imefundishwa kuanzia tarehe 13 / 05 / 2023 M mpaka leo 28/05/2023M.

Kazi iliyofanywa katika risala hii ni kutoa maana ya maneno ya kiarabu kwa kutumia maneno ya lugha ya Kiswahili (kufanya Tarjama) pamoja na kuongeza baadhi ya maneno ya ufafanuzi kwa ufupi.

Tunamuomba Allah ajaalie kazi hii iwe na utakasifu wa nia kwa ajili ya kutaraji uso wake na awanufaishe wasomaji na wasambazaji wa risala hii.

**Anasema Sheikh, ALLAH amrehemu:**

**'Pindi ALLAH anapomuamrisha mja wake jambo lolote ni wajibu juu yake (afuate) hatua saba (zifuatazo):**

1) **Elimu ya kulitambua lililoamrishwa.**

2) **Kulipenda lililoamrishwa.**

3) **Kuweka azma ya kweli ya kulifanya.**

4) **Kulifanya.**

5) **Ufanyaji wake uwe katika mwongozo wa sheria, uwe kwa utakasifu wa nia na ufuate mwenendo wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam.**

6) **Kutahadhari dhidi ya kutenda jambo lenye kuharibu tendo jema.**

7) **Kuthibiti imara (kudumu)"**

**Ufafanuzi mfupi:**

**Haya mambo saba ni lazima yawe vipaumbele vya kila mmojawetu katika safari yake ya kutekeleza maamrisho ya Allah Aliyetakasika na Aliyejuu , na pia katika kuepukana na makatazo yake. Sheikh ameyataja mambo hayo kwa kufuata mpangilio mzuri sana wenye kuzingatia umuhimu wa kitakiwacho kuanzwa kabla ya kingine kwa mujibu wa mafundisho ya dini yetu ya Uislamu. Ndio kusema ya kwamba, atakayeanza kutenda jambo aliloamrishwa na Allah Mtukufu kabla ya kulifahamu vema, basi hakika huyo ameruka hatua, yaani kaacha hatua ya awali itakiwayo kutangulizwa katika amri hiyo.**

**Kisha Sheikh, Allah amrehemu akaleta ufafanuzi wa hayo mambo saba baada ya kuyataja kwa ujumla akayaleta katika mfumo wa kuyachambua. Uchambuzi wake umebeba mifano kadhaa ya amri za Allah na makatazo yake sambamba na kuonyesha hali za watu katika kuyaendea maamrisho hayo na kujiepusha na makatazo hayo kwa mujibu wa hatua hizo saba kama ifuatavyo:**

**"Pindi mwanadamu anapofahamu kwamba Allah ameamrisha Tauhidi (kumpwekesha katika ibada) na amekataza Ushirikina ; au akafahamu kwamba Allah amehalalisha biashara na ameharamisha riba; au akafahamu kwamba Allah ameharamisha ulaji wa mali ya yatima kwa dhulma , na amehalalisha kwa msimamizi wa mali ya yatima ale (mali ya yatima) kwa wema endapo atakuwa fukara; ni wajibu juu yake alifahamu vema lililoamrishwa na aliulizie (kwa wajuzi) mpaka alifahamu vema, na (ni wajibu pia) alifahamu vema lililokatazwa na aliulizie (kwa wajuzi) mpaka atakapolifahamu vema.**

**Na lizingatie hilo kuwa ndio jambo la kwanza , yaani jambo la kumpwekesha Allah katika Ibada na jambo la kumshirikisha Allah…."**

**Ufafanuzi:**

**“ Kwa ufupi, Sheikh anaashiria kwamba; katika maamrisho na makatazo ya Allah, wanadamu wamegawanyika katika ufahamu wa aina kuu mbili zifuatazo;**

**1) Ufahamu wa ujumla.**

**2) Ufahamu wa upambanuzi.**

**Watu wengi wana ufahamu wa ujumla wa neno Tauhidi (upweke wa Allah katika Ibada) na uhalali wa kufanya biashara na mengineyo katika maamrisho ya Allah. Kama vile walivyo na ufahamu wa ujumla pia katika uharamu wa mambo mbalimbali ikiwemo Ushirikina na Riba, kwa kuwa ufahamu huo hauna msaada wowote kwa mtu ndio maana akatakiwa kila mmoja autafute ufahamu wa aina ya pili ambao ni ufahamu wa upambanuzi. Na huo ndio utakiwao kwa kila mmojawetu awe nao ili aweze kutenda maamrisho vema na kujiepusha na makatazo vema.**

**Na zingatia pale aliposema “na aliulizie (kwa wajuzi) mpaka alifahamu vema”, hapa anaonyesha namna ya kuupata huo ufahamu wa aina ya pili, ufahamu huo unapatikana kwa kusoma kwa wajuzi waliokuzidi maarifa ya dini yako ili uweze kupambanukiwa na maamrisho ya Mola wako pamoja na makatazo yake.**

**Kisha akaonyesha namna ambavyo wanadamu wengi hawapo tayari kuutafuta ufahamu wa aina ya pili na madhara ya hali hiyo kwao, kama ifuatavyo:**

**“ Na watu wengi wanafahamu (ufahamu wa ujumla) kwamba Tauhidi ni jambo la haki na Ushirikina ni jambo la batili, lakini wamepuuzia (kuutafuta upambanuzi) na wala hawaulizi; na (wengi wao pia) wamefahamu (ufahamu wa ujumla) kwamba Allah ameharamisha Riba lakini wakaendelea kufanya biashara pasina kuulizia (upambanuzi wa riba); na (wengi wao pia) wanafahamu (ufahamu wa ujumla kuhusu) uharamu wa kula mali ya yatima kwa dhulma na uhalali wa kula mali hiyo kwa wema, lakini wakaendelea kusimamia mali za yatima pasina kuuliza.”**

**Kisha akataja hatua inayofuata akasema:**

**“ Hatua ya pili:**

**Kulipenda lile ambalo Allah ameliteremsha; na (hupatikana) ukafiri kwa yule ambaye atachukia kile ambacho Allah amekiteremsha, kwa kauli yake Allah Mtukufu (( Hiyo ni kwa sababu walichukia kile ambacho amekiteremsha Allah , Allah akayaporomosha matendo yao)) Suurat Muhammad 9.**

**Na watu wengi hawampendi Mtume swallallaahu alaihi wasallam, bali wanamchukia na wanayachukia yale ambayo amekuja nayo hata kama wanafahamu kwamba hakika Allah ameyateremsha”**

**Ufafanuzi mfupi:**

**Baada ya kupata elimu ya upambanuzi wa jambo utakiwalo kulifanya katika sheria ya Mola wako, unalazimika kuipenda sheria hiyo ndani ya moyo wako. Mapenzi hayo ni lazima yapatikane kwa kuwa ndio alama ya kutukuzwa sheria ya Mola wako bali ndio sababu kuu itakayopelekea utendaji wako wa jamboi hilo uwe na faida na matunda kwako duniani pamoja na akhera.**

**Tambua kuwa mwenye kuichukia sheria ya Allah baada ya kuwa ameifahamu vema, huyo hana usalama mbele ya Mola wake, na matendo yake pia yapo hatarini kuporomoka kama alivyosema Allah ndani ya Qur'an kuhusu sifa na tabia za wale waliomkufuru: (( Hiyo ni kwa sababu walichukia kile ambacho amekiteremsha Allah , Allah akayaporomosha matendo yao)) Suurat Muhammad 9.**

**Mfano wa sheria za Allah zinazochukiwa na watu wengi ni mwenendo wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam , imefikia hatua mpaka kuchukiwa wale wenye kushikamana na mwenendo wake na kunasibishwa kuwa wameleta dini mpya. Yamebaki madai ya kumpenda Mtume swallallaahu alaihi wasallam kwa watu wengi yapo kwenye kutenda kinyume na mwenendo wake. Na mifano ipo mingi katika hili, baadhi ya mifano ni sherehe za kuzaliwa Mtume swallallaahu alaihi wasallam (Maulidi), usomaji wa khitma siku tatu au arobaini baada ya kuzikwa aliyefariki, usomaji wa albadiri na mengineyo.Yote hayo hayana mwongozo wowote na bahati mbaya anayefuata mwongozo wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam unaopingana na hayo anachukiwa na kuchukiwa sunna za Mtume swallallaahu alaihi wasallam. Ndio maana Sheikh akasema "Na watu wengi hawampendi Mtume swallallaahu alaihi wasallam, bali wanamchukia na wanayachukia yale ambayo amekuja nayo hata kama wanafahamu kwamba hakika Allah ameyateremsha."**

**Kisha akataja hatua inayofuata, akasema;**

**"Hatua ya tatu:**

**Kuweka azma ya kweli ya kutenda; wengi katika watu wanajua na wanapenda lakini hawaweki azma ya kweli ya kutenda , kwa kuhofia ubadilikaji wa (maslahi fulani ya) dunia yao."**

**Ufafanuzi mfupi;**

**Watu wengi tunashindwa kuweka maazimio na mikakati ya kweli na madhubuti katika kuyafanya mambo tuliyoamrishwa. Na hali hii ni miongoni mwa sababu za kushindwa kutekeleza mambo mengi katika sheria ya Mola wetu, hata yale mepesi mno yanakuwa mazito mno juu yetu, Allah atusaidie. Weka azma ya kweli ya kubadili mwenendo wako wa kiibada na kimuamala, anza leo usisubiri kesho, usihofie kwamba kuna jambo la kidunia utalikosa endapo utakuwa mwema!**

**Kisha Sheikh akataja hatua inayofuata, akasema:**

**“Hatua ya nne: Kutenda;**

**Na watu wengi wanapoazimia au wakaanza kufanyia kazi maazimio yao kisha wakaona kuna watu wanaowatukuza kama vile masheikh wao na wengineo, huwa wanaacha kutenda.”**

**Ufafanuzi mfupi:**

**Miongoni mwa maafa makubwa ni kuacha kutenda kheri na wema kwa sababu ya kuogopa macho ya yule unayemtukuza katika wanadamu wenzako, ambaye hapendi kukuona ukiwa katika wema huo. Pengine anaweza kuwa ni mtoto ambaye ameweka azma ya kuacha kutambikia mizimu , akahofia nafasi ya wazazi wake , akaacha kutekeleza azma yake akaingia tena katika ibada ya kuabudu mizimu. Hivyo, haitofaa baada ya kuwa una azma ya kweli ukaacha kuifanyia kazi azma yako kwa kuhofia nafasi ya mwanadamu mwenzako.**

**Kisha Sheikh akataja hatua inayofuata, akasema:**

**“ Hatua ya Tano:**

**Ufanyaji wake uwe katika mwongozo wa sheria, uwe kwa utakasifu wa nia na ufuate mwenendo wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam.**

**Hakika watu wengi wanaotenda wema matendo yao huwa hayawi katika utakasifu wa nia zao, na ikiwa yatatokea yakawa katika utakasifu wa nia, hayawi katika ufuataji wa mwongozo wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam.**

**Ufafanuzi mfupi:**

**Ametaja masharti mawili kwa Muislamu ili tendo lake jema liweze kukubalika mbele ya Allah Mtukufu;**

**1) Utakasifu wa nia (Ikhlasi).**

**2) Ufuataji wa mwongozo wa Mtume swallallaahu alaihi wasallam**

**Yote mawili yana nafasi sawa katika tendo lako jema, ukilipata moja ukalikosa jingine basi tendo lako halina nafasi ya kulipwa mbele ya Allah Mtukufu.**

**Kisha Sheikh akataja hatua inayofuata, akasema:**

**“ Hatua ya sita: Kutahadhari dhidi ya kutenda jambo lenye kuharibu tendo jema.**

**Hakika watu wema wanaogopa uporomokaji wa mema yao (baada ya kuyatenda); kwa kauli yake Allah; [ (Tahadharini) yasiporomoke matendo yenu mema hali ya kuwa hamjui ] Suurat Alhujuraat 2; Na hili jambo ni miongoni mwa mambo ambayo ni mara chache sana kuhofiwa katika zama zetu hizi.”**

**Ufafanuzi mfupi:**

**Hii ni hatua inayofuata baada ya tendo jema kufanyika, ni hatua ya msingi sana kwa sababu itahifadhi tendo lako ili libaki salama mpaka siku ya malipo. Endapo hatutachukua tahadhari dhidi ya matendo yaporomoshayo mema yetu , tutakuwa hatuna akiba yoyote ya wema siku ya malipo, tutakuwa mfano wa mtu ambaye atakwenda siku ya Qiyama hali ya kuwa alitenda duniani matendo mengi sana yaliyo mema lakini akayaporomosha, siku ya Qiyama yakafanywa kama vumbi litimkalo.**

**Kisha Sheikh akataja hatua ya mwisho, akasema;**

**" Hatua ya saba:**

**Kuthibiti imara katika haki na kuhofia mwisho mbaya, kwa kauli ya Mtume swallallaahu alaihi wasallam; (( Hakika miongoni mwenu kuna mtu atatenda matendo ya watu wa peponi, lakini atahitimishiwa kwa matendo ya watu wa motoni. )). Na jambo hili pia ni miongoni mwa yale ambayo watu wema huyaogopea sana , nayo ni mara chache mno kuogopwa katika zama zetu. Kutafakari kuhusiana na hali unayoifahamu kwa watu , katika hili na mengineyo , hukujulisha mengi sana ambayo ulikuwa huyajui, na Allah ndiye Mjuzi zaidi."**

**Ufafanuzi mfupi:**

**Matendo huzingatiwa mwishoni mwake, hivyo hakuna nafasi kwa muumini kubweteka na kujiliwaza kwa wema wake uliopita, kila mmoja adumu katika wema. Ikitokea ameteleza katika madhambi ainuke na atubie kwa Mola wake kisha safari ya kuendelea na wema iendelee.**

**Na aliposema Sheikh; "Kutafakari kuhusiana na hali unayoifahamu kwa watu , katika hili na mengineyo , hukujulisha mengi sana ambayo ulikuwa huyajui"; Anakusudia kuwa inawezekana kuna mtu unamfahamu alikuwa katika hali ya wema mwanzoni mwa umri wake lakini mwishoni mwa uhai wake akabadilika akawa muovo kupindukia kisha akafa katika hali hiyo. Wangapi walikuwa wakiswali, wakifunga swaumu za faradhi na hata za sunna, wakitoa sadaka na zaka katika mali zao na mengineyo katika mema, lakini baada ya muda fulani wakabadilika wakaacha wema wote waliokuwa wakiufanya na wakahamia katika uovu; wakawa wazinifu, wanywaji wa pombe, wachezaji wa kamari, na kadhalika; kisha wakafa katika hali hiyo.**

**Ukitafakari hali za watu hao utaona kuwa kila mmojawetu anayo nafasi ya kuiogopea nafsi yake isijekuangukia katika mwisho wa namna hiyo.**

والله أعلم

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم

**Kwa maoni na ushauri wako : 0683 758161**